# *Mwongozo Uliotolewa Na Mungu Wa Kuuendea Ushirika Wa Kiungu*

Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja katika Uwepo Wako wa Kiungu usiku wa leo, katika Jina la Bwana Yesu, Mwanao mpendwa, tukijitoa wenyewe, Bwana, Kwako kama dhabihu zilizo hai, tukijiweka wakfu kabisa kwa huduma Yako na kwa Injili Yako kuu katika siku hizi za mwisho, kama waaminio Wapentekoste, kama mwabuduo wa Mungu Mmoja wa kweli na aliye hai.

2 Jinsi tunavyokushukuru Wewe leo hii kwamba umetufanyia Kimbilio wakati wa shida, Mnara ambao tunaweza kukimbilia na kuwa salama! Dhoruba zinapovuma, na pepo ni kali, umeme ukimemetesha, hata hivyo, tunaweza kutulia tu hakika juu ya ahadi ya Mungu, kama vile mtoto mchanga angejisikia salama mikononi mwa mama yake. Tuna furaha sana kuwa na huo.

3 Tunakushukuru kwa ajili ya ushirika huu wa Full Gospel wa hawa wafanyabiashara, kwa ajili ya msimamo wao katika siku ya mwisho ya kuunganisha Mwili wa Bwana Yesu pamoja. Tunaomba, Bwana, ya kwamba mkutano huu daima utaendelea kupanuka mpaka tutakapoona kule Kuja kwa Bwana.

4 Tunamwombea Ndugu Oral Roberts, mtumishi Wako mwema. Na tunapoingia kwenye jengo hili usiku wa leo, na kuona kile imani ya mtu mmoja inaweza kufanya, tunakushukuru Wewe kwa ajili yake, Baba. Nasi tunaomba ya kwamba utabariki huduma yake, popote aendapo na yale afanyayo, na yafanikiwe mikononi Mwako.

5 Mbariki kila mhudumu aliye hapa, watoto wote wa Mungu. Mimina Roho Wako juu yetu usiku wa leo, na kutusahihisha na kutuingiza katika u—ushirika mkubwa kuliko tuliowahi kujua hapo awali pamoja na Yesu Kristo. Tujalie, Bwana, kwa kuwa tunaomba, katika Jina la Yesu, na kwa ajili Yake. Amina.

6 Ninataka kuchukua somo, usiku wa leo, la *Mwongozo Uliotolewa Na Mungu Wa Kuuendea Ushirika Wa Kiungu,* kuchukua hilo kama somo, kama ningeliliita hivyo. *Mwongozo Uliotolewa Na Mungu Wa Kuuendea Ushirika Wa Kiungu.*

7 Siku nzima, mimi. . .kila kitu kilionekana kuwa tofauti, siku fulani hii. Sijui, inaonekana kama, kuna nyakati kama hizo zinazokuja maishani, wakati watu wanapoanza tu kuona mambo tofauti kidogo na vile walivyoyaona wakati mmoja. Hii

ilikuwa ni siku isiyo ya kawaida, hali ya hewa hata ilionekana ya kushangaza, nilikuwa nikiona, kwa kuwa Biblia yangu ya kwanza niliyopata kujua ilikuwa ni maskini Mama Maumbile. Kama tu utafuata hayo, hutaenda kombo sana, ukiangalia maumbile, jinsi yanavyofanya kazi. Ilikuwa ni hayo, ndiyo yaliyoniongoza kwa Mungu, kujua ya kwamba kulikuwa na Mungu, nikiangalia maumbile.

8 Nilikuwa nikishuka mlimani, nikitazama huko kwenye Ziwa zuri la Umbagog, linaloelekeza kwenye Mto Androscoggin, niliona robini wote walionekana wakikusanyika na kufanya maskini mlio wa nyimbo zao. Mara kwa mara, ungesikia mkoromo kutoka kwa kulungu dume, na ilionekana kana kwamba walikuwa wakijiandaa kwa ajili ya jambo fulani, majira ya baridi kali yalikuwa yanakuja, nao walikuwa wakijiandaa kukusanyika.

9 Nilipokuwa nikipenya kupitia vikichakani nikakutane na rafiki yangu mahali tulipokuwa tumeegesha mtumbwi, kulikuwa na . . . alikuwa ameketi kwenye gogo, akingojea. Nami nikaona huko kwenye Ziwa Umbagog kundi kubwa mno la mabata, sijapata kuona wengi namna hiyo, ni vigumu, maishani mwangu, basi Bert, rafiki yangu, akasema, "Unaonaje juu ya hilo, Billy?"

10 Nikasema, "Vema, wanajiandaa kuruka kusini." Nikasema, "Hiyo ndiyo sababu jua lile lilitua alasiri ya leo, uliona vile, kabla halijatokezea juu ya mlima, jinsi lilivyoonekana jekundu sana? Theluji inakaribia, Bert, na namna fulani ya silika maalum ambayo Mungu ameweka katika uhai wa wanyama, wajitayarishe, kujiandaa kuondoka, wakati wa kuruka ujapo." Nikasema, "Hivi uliwaona hao ndege leo hii, na ro—robini, na kadhalika? Wanajiandaa kwa ajili ya safari yao ya majira ya baridi kali, pia. Kulungu wanajiandaa kukusanyika, kwa sababu kwamba dhoruba inakuja."

11 Basi tulipokuwa tukipiga makasia yetu ziwani na kuanza kuteremka, ninaamini kila bata kote juu na chini ya Mto Androscoggin alikuwa ameingia kwenye Ziwa Umbagog akijiandaa kuruka, na hayo makelele yote, kama tu mabata wanavyoweza kufanya, kupiga tu makelele, naye Bert akasema, "Unafikiri wanazungumzia nini, Billy?"

Nikasema, "Wana wakati mdogo wa ushirika kabla ya kuruka."

12 Ndipo basi, wakati mimi na Mhindi huyu rafiki yangu tulipokuwa tukishuka mtoni kwenye kambi yetu fulani, nao mwezi ukaanza kufifia, tukajua dhoruba ilikuwa inakuja, makasia yetu yakaanza kufanya mtibuko kidogo majini wakati huo, wakati mawimbi yakianza kupanda, nikawaza juu ya hili: "Hakika, wakati fulani kabla hatujaruka tutakuwa na wakati

wa ushirika, wakati makanisa yote yanaweza kukutanika mahali pamoja na yote yawe na wakati wa ushirika kabla hatujaruka."

13 Basi miaka ikapita, nilikuwa mchungaji wa Kibaptisti wa eneo hilo wakati huo huko Jeffersonville, na—na kadiri miaka ilivyopita, nikaingia katika Ushirika huu mkuu wa Wafanyabiashara wa Full Gospel, ndipo nikaanza kuona jinsi ambavyo wangetumia pesa zao, na kwenda mahali mahali na kukutana kote nchini, naam, na ulimwenguni, ndipo walipokutana, hapakuwapo na tofauti kati yao. Hawakuwa ati mmoja, akisema, "Mimi ni mshiriki wa kusanyiko fulani hili," na mwingine, kusanyiko fulani. Wote walikuwa na mambo shirika. Kwa hiyo nikafikiri hapana shaka hilo ndilo nililokuwa nikiwazia usiku huo, juu ya ushirika, kukusanyika pamoja kabla kule kuruka hakujaanza.

14 Sasa, niliwaona pale, katika uamsho huu mkuu, wa Kipentekoste, hapakuonekana kuwapo na hukumu yoyote miongoni mwao. Ukikutana nao kwenye chumba cha hoteli, watakumbatiana moja kwa moja mbele ya—ya watu mashuhuri, ama chochote kile, na kukumbatiana, na kumsifu Bwana, na kulia kidogo, na kupaza sauti kidogo, na kutenda tu kama wafanyavyo mahali pengine popote, nami nikawazia, "Mnajua, hilo ni halisi, hilo ni, kuna jambo fulani kuhusu hilo," wanawake, vivyo hivyo. Ilionekana tu kuwa ni ushirika mkuu.

15 Nami nikashangaa, "Nashangaa ni kitu gani kinachosababisha hayo, na ni kwa nini sisi sote hatuwezi kufanya hivyo? Ni kwa nini watu wote, wanadamu wote, hawawezi kujisikia hivyo? Hakuna hukumu, huru tu uwezavyo kuwa." Nikawaza, "Vema, kwa nini kila mtu asiwe hivyo?"

16 Sasa, ninaamini tunaweza, lakini kuna . . . Na sababu ya sisi kufanya hivyo kwanza ni kwa sababu kuna kitu fulani katika maisha ya mwanadamu kinachotamani jambo hilo, kitu fulani kinacholiitia.

17 Leo kwenye ndege, nikija huku kutoka Louisville hapa chini, mimi . . . ilinichukua saa mbili na nusu kuruka, ikanichukua siku nzima kufika, kuchelewa kwa ndege. Na labda Mungu alihusika nalo. Nilipofika Louisville, kulikuwa na msichana aliyepanda hiyo ndege na kuketi karibu nami, naye akasema, "Unajali kama nikiketi hapa?"

Nikasema, "Hata kidogo." Ndipo tulipokuwa tukiendelea, walikuwa wakiandaa chakula cha mchana kwenye ndege, nami nikaomba.

Naye akasema, "Je, wewe ni mhudumu?"

Nikasema, "Naam, mama, ndivyo nilivyo."

Naye akasema, "Mimi pia ni mwaminio." Naye akaniambia juu ya dhehebu lake fulani.

Nikasema, "Hilo ni zuri."

18 Ndipo nikaona tulikuwa na kifurushi kidogo cha sigara kwenye ndege, nami nikaangalia nione kile angefanya juu yake. Kwa hiyo mara tu chakula cha jioni kilipokwisha, alianza kukifungua kifurushi hicho cha sigara, naye akapapasa-papasa moja kidogo, kisha akaielekeza kinywani mwake, kisha akaishusha tena, ndipo baada ya kitambo kidogo akaiwasha. Akasema, "Hujali kama nikivuta sigara?"

Nikasema, "Hujali kama nikikwambia ninajali?" Nikasema—nikasema, "Ni—ni—ninajali, kwa sababu. . . "

Akasema, "Kwa nini?"

Nikasema, "Siwezi kuelewa ni kwa nini maskini msichana mzuri, mwenye haiba uliyo nayo ingembidi kufanya jambo kama hilo."

Akasema, "Loo, ninapata utoshelevu kutokana nayo."

19 Nikasema, "Huo ni utoshelevu mbadala tu. Kama ungechukua tu yale ninayokwambia, na ungemtolea Mungu maisha yako kabisa, umepungukiwa na *kitu fulani*, nawe unajaribu kufanya sigara ziridhishe hiyo shauku iliyo moyoni mwako, zikupe utoshelevu wa uongo, ambao hivi karibuni zitakupa kansa ama kuudhalilisha mwili wako, nawe utakwisha."

20 Ndipo nikasema, "Mungu alimfanya mtu kuona kiu, kumwonea Yeye kiu, ndipo wasipokubali hilo, basi ibilisi anawapa dhana potovu ya raha, nao wanajaribu kuiridhisha kwa mambo ya ulimwengu."

21 Alikuwa amevuta hiyo sigara yapata mara mbili, akasema, "Nina umri wa miaka ishirini na miwili," akasema, "mvulana mchumba wangu mpenzi ana umri wa miaka thelathini na miwili." Kasema, "Aliniambia, nimekuwa ng'ambo miezi mitatu, akanisihi nisivute sigara tena." Kisha akasema, "Hii ndiyo mara ya kwanza nimevuta sigara, nikikosa ndege." Naye akasema, "Bwana, ninachukua ahadi hii sasa," akaizima sigara, akachukua. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

22 Mungu anapenda kufanya ushirika pamoja na kiumbe Chake. Katika bustani ya Edeni tunaambiwa, kwamba wakati mwanadamu alipotembea katika unyofu wa Mungu, Mungu alishuka wakati wa jua kupunga na kufanya ushirika na watoto Wake. Ndipo, siku moja kulikuwako na sauti iliyotokea Mbele za Mungu, na kusema, "Hao, wapendwa Wako, watoto Wako, wameanguka, nao wametenda dhambi na wamefanya mabaya."

23 Mwajua, Mungu hakumchagua tu Malaika fulani ashuke chini na kuchunguza aone kama ndivyo ilivyokuwa ama sivyo, ama Kerubi fulani wa Mbinguni, bali Mungu alikuja Mwenyewe, akilia, "Adamu, uko wapi?" Mungu, Mwenyewe, akaja akimlilia mtoto Wake aliyepotea. Alipomwona amejificha vichakani, nyuma ya majani ya mtini yaliyoshonwa, Yeye alisema, "Ni

nani aliyekwambia, ulikuwa uchi?" Wala asingeweza kutoka na kufanya ushirika tena na Mungu.

24 Sasa, kama kuna ushirika wa kweli . . . Naye Mungu ni upendo, na upendo unadai ushirika. Kama vile mume na mke vijana, wakati mvulana anapokutana na msichana, naye anamwambia . . . anafikiri yeye ni mrembo sana, na—naye anampenda, wanataka kufanya ushirika, ushirika halisi. Lakini kabla hawajaweza kufanya ushirika huu, hapana budi pawe na maafikiano, kabla hawajaingia katika arusi, ndoa, hapana budi pawe na maafikiano kwa ajili ya ushirika huu fulani. Nao umewekwa msingi juu ya makubaliano ya nadhiri zao mmoja kwa mwingine, na kisha ndoa takatifu, ndipo basi tunaingia katika ushirika wa maisha. Lakini kabla hatujaingia katika ushirika huo, hapana budi pawe na maafikiano kwanza.

25 Basi wakati ushirika ulipovunjwa kati ya Mungu na mwanadamu, ilibidi kuwe na maafikiano ya namna fulani, namna fulani ya mipango ya kurejesha tena ushirika huo uliopotea. Ndipo Mungu akapata huo mpango, nao ulikuwa ni kwa damu ya mhanga asiye na hatia ambapo Mungu alimrejesha mwanadamu katika ushirika pamoja Naye tena.

26 Kumekuwa na vibadala vingi vilivyojaribiwa, Adamu alivijaribu, tumejaribu kuwaelimisha watu kwake, tumejaribu njia zote mbalimbali, bali hakuna kitu kinachomrudisha mwanadamu katika ushirika pamoja na Muumba Wake ila Damu ya Mwanawe, Yesu Kristo. Ndilo toleo pekee alilo nalo Mungu, ni Damu.

27 Mhanga asiye na hatia alikufa kwa ajili ya mtu mwenye hatia, ambaye alirejesha ushirika wa Mungu na mwanadamu tena, ndipo Adamu, akifunikwa na damu hii, angeweza kusimama mbele za Mungu na kuabudu tena. Loo, ninapenda hilo! Kuna jambo fulani kulihusu, unaponena juu ya damu! Damu ina uhai. Pasipo kumwaga damu hakuna ondoleo la dhambi.

28 Unaweza kuwa na kila kitu ulimwenguni, unaweza kuwa na kitu chochote unachotaka, kitu chochote cha kuabudu, kanuni yoyote ya imani ya kuishia, bali kamwe huwezi kuingia katika ushirika, ushirika wa Kiungu pamoja na Mungu, mpaka kwanza uje chini ya Damu. Hiyo ndio njia takatifu ya Mungu, na iliyokusudiwa, na iliyowekewa wanadamu kufanya ushirika Naye, kupitia Damu ya Mwanawe, Bwana Yesu Kristo. Huo ulikuwa ni mpango wa Mungu, ungali ni mpango wa Mungu, utakuwa ni mpango wa Mungu milele, hakuna mpango mwingine ila kwa kumwagwa kwa damu.

29 Agano la Kale, safarini, Israeli kutoka kwenye nchi ya uenyeji wao, wakivuka, ama kutoka Misri, hasa, wakienda kwenye nchi za uenyeji wao, wakienda zao kule, Mungu alifanya maandalizi kupitia damu.

30 Tunataka kuwazia sasa juu ya mlango wa 19 wa Hesabu, Mungu alimwambia Musa na Haruni, "Nendeni, mkamtwae ndama mwekundu," sasa, ishara nyekundu, mara nyingi ni rangi mbaya au hatari, lakini nyekundu pia inamaanisha upatanisho, "nendeni mkamtwae ndama mwekundu, mwekundu mwili wote, asiye na doa juu yake." Yeye alimwakilisha, bila shaka, Kristo. Na ndama huyu kamwe asiwe na nira kamwe shingoni mwake. Kama alipata kufungwa nira, basi a—amehukumiwa, hapaswi kufungwa nira pamoja na ulimwengu.

31 Hivyo ndivyo Kanisa lilivyo siku hizi. Kristo, wakati alipokuja, hakujifunga nira pamoja na ulimwengu, alikaa pamoja na Mungu, wala hakufungwa nira pamoja na ulimwengu. Kanisa linalomwabudu Mungu siku hizi, limefungwa nira pamoja na Kristo, chini ya Damu.

32 Ndipo tunaona ya kwamba ndama huyu alipaswa kuuawa wakati wa jioni mbele ya kanisa lote. Eleazari alikuwa atwae damu yake kwa vidole vyake, na kutembea kuelekea mlangoni pa maskani, na kuinyunyiza hiyo damu mara saba, ama vinginevyo, kuweka milia saba juu ya mlango wa kusanyiko. Ndipo huyo ndama alipaswa kuchomwa moto, kwato, pembe, ngozi, nyama, na yote. Na katika huku kuteketezwa kwa huyo ndama, alipaswa kuchanganywa na hisopo (*Hisopo*, ninaamini ndilo neno bora zaidi kwake, linatamkwa hivyo.), hisopo, nyekundu, na mti wa mwerezi.

33 Sasa, nyekundu katika Maandiko ilikuwa sufu kutoka mgongoni mwa kondoo dume iliyotiwa rangi nyekundu, ikiwakilisha Mwana-kondoo aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ilikuwa ichanganywe katika haya, kwa sababu haya yangekuwa ni maji ya farakano ya kumtakasa mwabudu asiye safi, apate kuwasilishwa Mbele za Mungu.

34 Tunaweka msingi gani? Tunajaribu kutafuta njia halisi, ya kweli ya ushirika halisi pamoja na Mungu. Tumejaribu kufanya mambo ya kila namna kulifanikisha, kuelimisha, kuunda madhehebu, bali kuna mpango mmoja tu wa Kiungu, huo ni ile Damu. Nje ya hiyo Damu hakuna ushirika, hakuna hata utakaso wa dhambi mpaka tuifikie Damu.

35 Sasa angalieni, ndipo sufu hii, iliyotiwa rangi nyekundu, iliwakilisha kondoo dume wa Habili ambaye alimtolea kwenye lile jiwe kubwa bustanini, nje ya bustani ya Edeni kwa ajili ya dhambi zake, wakati alipokishika maskini kichwa chake, na kukirudisha nyuma, na kukikata kwa kipande cha mwamba, sidhani walikuwa na visu au mikuki siku hizo, akakata maskini koo lake, mpaka damu ikatiririka kwenye maskini sufu yake yote, naye akafa akilia, akiomboleza.

36 Ilikuwa mfano wa Mwana wa Mungu, miaka elfu nne baadaye, ametundikwa msalabani, akitokwa na damu, nywele Zake, akitokwa na damu, Naye alikuwa akifa, akilia, "Mungu

Wangu, Mungu Wangu, mbona umeniacha?" Hiyo ilikuwa ni ile sufu nyekundu iliyotiwa ndani ya maji ya farakano.

37 Halafu mti wa mwerezi, mwerezi ni nyekundu juu ya nyeupe. Nyekundu kupitia nyekundu hufanya nyeupe, ukiangalia kupitia kitu chekundu kwenye kitu chekundu, kinafanyika cheupe. Mfano, kwamba wakati Mungu anapoangalia kupitia Damu nyekundu ya Mwanawe, Bwana Yesu, dhambi zetu nyekundu, nyekundu sana, zinakuwa nyeupe kama theluji. "Nioshe katika Damu, nami nitakuwa mweupe kama theluji." Hakuna kitu kingine ungaliweza kuwa nacho. Ninauthamini ule wimbo wa kale wa Jeshi la Wokovu:

> Loo, huo mtiririko ni wa thamani,
> Unaonifanya mweupe kama theluji;
> Sijui chemchemi nyingine,
> Ila Damu Yake Yesu.

38 Hiyo ndiyo Chemchemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, wakati wenye dhambi wanapotumbukizwa chini ya gharika hiyo, hupoteza madoa yao yote ya hatia.

39 Nyekundu kupitia nyekundu, na kisha hisopo: Nilipata, nikitafuta nione hisopo ilikuwa ni nini, hisopo ni gugu la kawaida tu linalopatikana Misri, na pia linapatikana Pa—Palestina. Na wakati mwingine inakulia kwenye kuta ambako uchafu . . . Ni gugu tu la kawaida, la kawaida, jani dogo juu yake lenye ua dogo, jeupe.

40 Nayo hisopo sikuzote ilitumiwa kunyunyizia damu. Katika siku za Pasaka, Musa aliamuru wachukue hisopo, na kuichovya katika damu, na kuinyunyizia kwenye mwimo wa mlango na kwenye vizingiti, kuipaka hiyo damu.

41 Nayo hisopo, ikiwa ni gugu la kawaida tu, katika maji haya makuu ya farakano, inawakilisha imani ya kawaida. Mwaminio akija, hapaswi kuwa wa kimbinguni, loo, Mimi-sijui-nini, jamaa wa namna fulani ambaye ana elimu ya juu sana hata a—ana . . . anajua yote, zaidi ya Webster ajuavyo, wala si lazima awe mwanatheolojia yeyote mashuhuri, hana budi tu kutumia imani ya kawaida, hisopo, aiokote popote.

42 Na vyote vilichanganywa pamoja na kuchomwa moto. Ndipo basi viliwekwa nje ya nyua ambapo mtu najisi, kabla hajaweza kuingia katika ushirika . . . Basi kumbukeni, Mungu siku zote alikutana, wala kamwe si mahali pengine popote, ila alikutana na mwanadamu chini ya damu. Hapo ndipo mahali pekee unapofanya ushirika na Mungu ni chini ya Damu, mnakaribia tu mpaka mtakapofikia mahali hapo.

43 Israeli wote walikusanyika ambapo mwana-kondoo wa dhabihu alichinjwa, na chini ya damu hiyo walifanya ushirika, nje ya damu, hapakuwapo na ushirika. Daima umekuwa mpango wa Mungu uliowekwa kukutana na mwanadamu chini ya damu, ni kwa kuwa Yeye humwangalia mwanadamu kupitia damu na

kumwona ni mweupe, nje ya hiyo, yeye ni mwenye dhambi. Hakuna kitu, usingeweza kujisafisha mwenyewe, hakuna kitu ungaliweza kufanya kujifanya bora zaidi. Huwezi kufanya marekebisho, na kadhalika, kufanya ninii moja . . . Ni kama tu chui akijaribu kujiondolea madoa yake kwa kuyalamba, kunayafanya tu maangavu zaidi.

44 Na mawazo yetu yote ya kujibunia kwamba sisi ni wazuri tu kama mtu mwingine, sivyo mpaka tutakapokuja chini ya Damu ya Bwana Yesu Kristo. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Hiyo ni kweli. Hapo ndipo mahali pekee pa Mungu pa kukutania na mwanadamu, chini ya Damu.

45 Ndipo wakati Israeli walipofikia mahali pa kuabudia, wote wakienda . . . ndipo mtu aliyenajisika alipokuja kwanza, ilibidi aje kwenye nyua za nje. Nayo damu hii, ama, maji haya ya farakano, ambayo yanaitwa na Agano Jipya, tunaoshwa kwa Maji ya Neno. Maji ya Utengano ni Neno la Mungu. Imani chanzo chake ni kusikia. Basi mtu huyu akiingia alinyunyiziwa maji haya ya farakano.

46 Ndipo kama vile mwenye dhambi anavyoingia na kuisikiliza Injili, anaanza kutambua hukumu. Yeye ni mwenye dhambi, anatambua ya kwamba katika maji haya ya farakano kuna rangi nyekundu, mtu fulani alimfia, kibadala kisicho na hatia, kumleta katika ushirika na uhusiano na Mungu tena. Alitambua jambo hilo, ya kwamba ameondoka njiani kwa kuhubiriwa kwa Neno. Ninasema hivi: Kwamba Injili, ingawa katika urahisi wake, ikihubiriwa katika nguvu za ile Damu, ndiyo kivutio kikuu sana ulimwengu ulichopata kujua.

47 Mataifa yana njaa ya mamlaka siku hizi. Niliona wakati fulani uliopita ambapo petroli fulani, chini ya hali fulani ya masharti fulani ya kubainisha, ingeinua Sfiniksi kutoka ardhini futi mbili, nao walikuwa wanajivunia petroli yao.

48 Nilikuwa nikisoma gazeti kwenye ndege, nami nikalitupa nyuma, na kusema, "Naam, lakini Mungu asifiwe, ninajua kitu Fulani chenye nguvu zaidi ya hiyo, kwamba matone mawili ya Damu ya Yesu Kristo yatamwinua mwenye dhambi aliyepotea na amekwisha, yamtoe kahaba mtaani na kumfanya mtakatifu, yamtoe mlevi kutoka kwenye mifereji ya maji taka huko nje na kumfanya mtakatifu wa Mungu, mhubiri wa Injili."

49 Hizo ndizo nguvu za tone moja la Damu ya Bwana Yesu. Amina. Hilo ndilo ulimwengu unalohitaji kujua, mamlaka leo.

50 Mungu anayo njia iliyowekwa. Na wakati Mmataifa, ama mtu mchafu alipotamani ushirika na Mungu, jambo la kwanza lililombidi kufanya, lilikuwa ni kuja, kwanza, kwenye maji ya farakano, kisha anyunyiziwe.

51 Sasa, hiyo iliwakilisha au kufananisha nini? Mwaminio siku hizi, mtu anayetaka kuamini, anakuja kanisani, na kuisikiliza Injili: Kristo alikufa kwa ajili ya wenye dhambi. Mle ndani,

nyekundu, sufu nyekundu, hisopo basi, anatumia hiyo kwa imani ya kawaida ambayo m—mtoto wa miaka miwili angeweza kutumia. Kumwamini tu Bwana Yesu Kristo.

52 Kuna mengi sana siku hizi, kuna wengi wetu sana, kama mtu fulani akisema, "Nifanye nini nipate kuokolewa?"

"Achana na udanganyifu wako, achana na wizi wako, achana na uvutaji wako sigara, achana na unywaji wako pombe."

53 Ninaamini wanapaswa kufanya hivyo, pia, lakini hilo halijibu swali lake, unamwambia cha *kutofanya*, anataka kujua la *kufanya*. Paulo alimwambia yule mlinzi wa gereza la Filipi, kamwe hakumwambia "Rudisha upanga wako, kisha ufanye *haya* yote, na *mengineyo*," alisema, "Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe utaokoka, wewe pamoja na nyumba yako. Amini, kuwa na imani."

54 "Ninawezaje kuwa na imani hiyo, Ndugu Branham?"

55 Ni rahisi tu kama kufikia, kuchukua hisopo kupaka damu. Liamini kwa ajili yako mwenyewe, amini ya kwamba Kristo alikufa kwa ajili yako, amini ya kwamba Yeye alikuwa Ndiye asiye na hatia aliyekufa mahali pako kama mwenye dhambi, na mwenye hatia. Vivyo hivyo na uponyaji wa Kiungu, imani rahisi tu ya kuamini Neno Lake. Loo, wanajaribu kulifanya gumu, wanajaribu kulifanya kubwa sana.

56 Hiyo ndiyo sababu ule uamsho mkuu ulitokea huko Uingereza. Kanisa la Kianglikana lilikuwa limelifanya gumu sana, wenye elimu pekee ndio wangeweza kulielewa. Naye Mungu, kanisa linapoingia katika hali hiyo, Mungu sikuzote hutuma uamsho wa urahisi, na kukivunja kitu hicho vipande-vipande. Hiyo ni kweli.

57 Hicho ndicho tunachohitaji siku hizi ni ule urahisi. Huo ndio taifa linaohitaji siku hizi ni urahisi wa imani katika Kristo kujisalimisha wenyewe bila ubinafsi kwa moyo wao wote, nafsi, na akili, na yote waliyo nayo kwa Bwana Yesu. Rahisi tu, haikubidi kujifunza chochote hata kidogo, amini tu ya kwamba Yesu alikufa apate kukupa baraka, basi ni yako kwa imani. Mara unapochukua hiyo imani-ya hisopo na kupaka damu, jambo fulani linatukia katika moyo wa kila mwanamume, ama mwanamke, anayefanya hivyo. Amina.

58 Ninajisikia kubarikiwa sasa hivi. Naam, bwana, kwa sababu ninajua ya kwamba hiyo ni kweli. Kama iliniokoa, itamwokoa mtu yeyote, Damu ya Yesu Kristo.

59 Hapa miaka kadhaa iliyopita walizikutanisha dini za ulimwengu. Nilikuwa nikisoma hilo kwenye kitabu, walikuwa na huyu Bibi Maccabee kutoka Oklahoma, hapa, ambaye alikamatwa hapa nje kwenye. . .huenda ilikuwa huko Tulsa, ama moja ya sehemu hizi. Alikuwa akikimbia mtaani,

akiendesha gari la farasi la abiria, akivuta msokoto, akivunja kikomo rasmi cha spidi ya gari lake la farasi la abiria.

60 Basi wakati hao, dini zote, dini mbalimbali zilipoinuka na kusimulia sehemu zao za dini yao, jinsi ilivyokuwa kuu. Imamu wa Kiislamu akasimulia jinsi dini yake ilivyokuwa kuu, Mbuddha akaelezea jinsi dini yake ilivyokuwa kuu, ndipo maskini mhudumu fulani, siwezi kukumbuka jina lake sasa, alikuwa akiwakilisha dini ya Marekani, dini ya Kikristo.

61 Basi alipopata nafasi yake jukwaani, alisimulia hadithi ya mwanamke huyu mashuhuri, wa kuchukiza, jinsi alivyokuwa duni sana hata wao hawakutaka kumkaribia hata kumkaribia vya kutosha kummwagilia lami na kumtia manyoya, alikuwa mtovu wa uadilifu sana, alikuwa duni sana, hakuna kitu kingaliweza kumsaidia, ndipo akasema, "Enyi waungwana wa dini za ulimwengu huu, je, dini zenu zinaweza kutoa chochote ambacho kingesafisha mikono ya mtu huyu mwovu?"

Kila mtu aliketi kimya, moja kwa moja mwishoni mwa viti vyao, hakuna mtu aliyesema chochote.

62 Ndipo akaruka hewani na kupiga mayowe na kugonganisha visigino vyake pamoja, kasema, "Damu ya Yesu Kristo haitasafisha tu mikono yake, bali itausafisha moyo wake na kumfanya safi kama yungiyungi."

63 Damu ya Bwana Yesu Kristo huondoa dhambi, na kutusafisha na uovu wetu wote, na kutufanya viumbe vipya katika Kristo Yesu. Hakuna kitu kingine kitakachofanya hivyo, kanuni za imani, taratibu, wala chochote kile kitakachochukua mahali pake, kimejaribiwa, bali inahitaji hiyo Damu.

64 Hapo ndipo mahali pekee pa ushirika wa Kiungu, ni chini ya Damu. Hiyo ndiyo tiba pekee anayoijua Mungu. Aliliwekea msingi . . . Yeye hana kikomo, yale anayosema kwanza, hana budi kudumu nayo sikuzote katika mpango Wake.

65 Sasa, watakapokuja nyuani, wakitambua ya kwamba wametiwa unajisi, wakiketi katika kusanyiko, wakijua wamekosea, kwa imani wanajipaka hiyo Damu, wanaiamini, wanaikubali, yale maji, kuoshwa kwa maji kwa Neno, kunawasafisha basi na kuwafanya tayari.

66 Sasa, hapa ndipo hilo jambo linapokuja, hapa ndipo hiyo hoja inapokuja. Watu wengi husema, "Ninapoamini, hilo tu ndilo ninalopaswa kufanya." Sasa, hapo ndipo msuguano unapoingilia, mtu aliyeyafikia maji ya farakano *asingeweza* bado kuingia katika Patakatifu pa patakatifu, bado *asingeweza* kuingia kwenye kusanyiko.

67 Aliyakubali, akayaamini, na kuamini yalikuwa ni kwa ajili yake, naye akanyunyiziwa maji ya farakano, lakini alipokuwa akisafiri kuelekea mahali pa ushirika, kitu cha kwanza kilichombidi kukabiliana nacho, pale mlangoni, kilikuwa ni ile

milia saba ya nyakati saba za kanisa, Mungu katika nyakati zote, ni damu pekee, naye ilimbidi ajue ya kwamba dhabihu ilimtangulia, ikitokwa na damu. Ilimbidi kuitambua ile damu kabla hajaweza kuingia katika kusanyiko.

68 Sasa, basi alipokuja chini ya damu hii, ndipo akaingia katika kusanyiko, katika Uwepo wa Utukufu wa Shekina wa Mungu ndipo basi akawa katika ushirika mkamilifu, akiabudu chini ya damu. Ni picha nzuri jinsi gani ya Kristo wakati wa Pentekoste, akiliingiza Kanisa Lake katika ushirika mkamilifu!

69 Ni kama wale mume na mke vijana niliokuwa nikizungumzia, wanapofunga ndoa, hilo silo jambo lote, hawajafanya chochote ila kufanya sherehe, mhudumu amesema tu, "Ninawatangaza ninyi mume na mke." Haiko tayari bado. Anafanya nini? Anampeleka kwenye nyumba yake aliyomwandalia.

70 Sasa, watu wengi hapa huenda wasikubaliane nami kwa hili, bali huishi ila katika nyumba ya vyumba vitatu tu. Loo, huenda ukawa na vyumba vingine vingi, lakini kweli una vyumba vitatu tu, yaani jikoni, sebuleni, na chumba cha kulala. Huenda ukawa na vyumba vitatu au vinne vya kulala, na huenda ukawa na jikoni, na chumba cha kulia chakula, na kadhalika, lakini kwa kweli mtu anaishi tu katika nyumba ya vyumba vitatu.

71 Unaishi katika nyumba yenye vyumba vitatu mwilini mwako: nafsi, mwili, na roho. Mungu aliishi katika nyumba yenye vyumba vitatu: Baba, Mwana, Roho Mtakatifu. Kila kitu kiko katika tatu. Na tatu ni pembetatu.

72 Chukua pembetatu na uimulike, vema, ambapo tatu zinakutana mahali pamoja, zitatoa rangi saba mbalimbali. Rangi saba mbalimbali ni upinde wa mvua, upinde wa mvua ni agano. Loo, linaendelea tu kwenda mbele, zaidi, na zaidi, na zaidi! Linaendelea, kwa kuwa, Mungu alifanya agano kupitia vitu hivi vitatu: hisopo, sufu nyekundu, na kadhalika. Nayo Nuru ya Mungu ikiangazia hili, inafanya agano, agano ambalo Mungu alifanya.

73 Sasa, wakati mwanamke anapoletwa, bibi-arusi kijana, loo, jinsi anavyompenda, lakini hata hivyo, wao hawako kweli katika ushirika mkamilifu bado. Sasa jambo la kwanza: Jikoni ni pa kufanyia nini? Ni mahali unapokula.

74 Hivyo ni kama ilivyo katika nyua za kwanza za kanisa. Unakula hapa, unakuja, unaketi kwenye kiti cha nyuma, unalisikiliza Neno, na muda si muda wajua unaanza kusema, "Ee Mungu, hilo lilimaanisha mimi!" Unamkubali kama Mwokozi wako binafsi, kwa imani unalishika, ndipo unaanza kula Neno.

75 Unaanza ku—kujisikia ya kwamba umemkubali Kristo kama Mwokozi wako binafsi. Unaanza kula Neno, unalifurahia, ambapo, ulikuwa, ungeamka na kutoka nje ya jengo kama

mhubiri hakusema jambo lililokufaa kabisa, lisilo sawa, ungeamka na kutoka nje. Lakini ukiisha kumkubali Kristo wakati mmoja, umetengwa basi, maji kwa Neno la utengano yalikutenganisha na mawazo yako maovu.

76 Ndipo jambo linalofuata ni kuingia se—sebuleni ambamo unampeleka maskini bibi-arusi wako. Anaondoa utaji wake, unamkaribia kidogo, ndipo unapomkaribia, unamkumbatia, unazungumza naye, unamkumbatia.

77 Hivyo ndivyo ilivyo katika ushirika wa Bwana Yesu. Kabla hujafanya hivyo, unatengwa na dhambi zako, ndipo unaikumbatia Injili ya Bwana, unalikumbatia Ne—Neno lililoandikwa, unaliamini kwa moyo wako wote. “Mungu, haijalishi kile unachotaka nifanye, chochote ulichopanga maishani mwangu, niko tayari sasa kukipokea.” Hiyo ni se—sebuleni.

78 Halafu, bado unasema, “Huu si umbali wa kutosha?” La, bwana.

79 Chumba kinachofuata ni chumba cha kulala. Ndipo unapoingia kwenye chumba hiki cha kulala, basi ni, unaingia katika ushirika na uhusiano. Unaingia katika uhusiano, ndipo unakuwa na ushirika mkamilifu, kwa sababu huwezi kuwa na ushirika mkamilifu mpaka uwe na uhusiano, mtu yeyote anajua hilo.

80 Basi sikilizeni, ndivyo ilivyo kwa kanisa siku hizi, tuna watu wengi kupita kiasi, tuna wengi kupita kiasi ambao wanaona aibu kuingia katika uhusiano mkamilifu pamoja na Mungu kwa maisha mapya na kuzaliwa upya. Kama sisi ni Bibi-arusi wa Kristo, basi kwa nini hatuwezi kuingia katika uhusiano? Ndipo aibu yote na kurudi nyuma na yote yametuondokea.

81 Kama tukiingia katika uhusiano mkamilifu, tumezaliwa mara ya pili, sijali, Rais wa Marekani angeweza kuwa amesimama mtaani, ungepaza sauti, “Haleluya! Bwana asifiwe! Haleluya!” Hujali, kwa sababu umeingia katika uhusiano, umezaliwa mara ya pili, wewe ni mtoto mpya, uko katika Utukufu wa Shekina pamoja na Mungu, ukifanya ushirika pamoja Naye. Hivyo ndivyo ninii. . .Tunachohitaji leo, ndugu, ni ibada chini ya Damu, ibada yenye uhusiano mkamilifu tupate kufa.

82 Vipi kama maskini bibi-arusi alisema, “Sasa ngoja kidogo, Ni—ni—ninaninii tu, sijui, sikujua ya kwamba maisha ya ndoa yana mambo kama hayo”? Kamwe asingeingia katika ushirika pamoja na mumewe. Asingeweza kamwe kuingia katika uhusiano, ama, ushirika mpaka kwanza aingie katika uhusiano.

83 Hiyo ndiyo shida ya kanisa siku hizi, wanasema, “Loo, siamini kwamba kuna namna fulani ya dini inayokufanya upaze sauti, na kuiita ‘dini ya moyoni,’ wala, siamini mambo kama hayo.”

84 Si ajabu, hujawahi kuingia ndani yake bado. Ukiingia ndani yake na kweli uingie chini ya Utukufu wa Shekina wa Mungu, wakati nguvu za Roho Mtakatifu zinaposhuka juu yako, utajua jambo fulani limekupata, kwamba umepita kutoka mautini kuingia Uzimani, na umekuwa kiumbe kipya. Unamtanguliza Mungu.

85 Vipi . . .? Ilikuwa ni Charles Finney wakati huo aliyetoa tamshi kuhusu jinsi alivyokuwa . . .? Alikuwa . . . Ninaamini ilikuwa ni Charles Finney, ambaye, alikuwa akihubiri, ama mtu fulani, huenda haikuwa ni yeye, ndiyo kwanza niisome mahali fulani, ya kwamba alikuwa akihubiri, alikuwa na mahubiri, na maskini wanawake wawili walikuwa wakimwombea kwamba apate Roho Mtakatifu, naye akawaambia alikuwa na Roho Mtakatifu.

86 Basi siku moja alitoka akaenda nyuma ya, ofisi yake kuomba na kupiga magoti ambapo mti wa kale ulikuwa umeanguka, basi wakati alipokuwa akiomba, mbona, kijiti kilivunjika naye akafikiri mtu fulani alikuwa anakuja, ndipo akaruka juu, akasema, "Ahem! Ahem! Ahem!" Akaangalia pande zote. Alidhani mtu fulani alikuwa pale, na kumwona akiomba.

87 Ndipo akaketi chini na kusema, "Kama ningekuwa nikizungumza na bosi wangu ofisini, ningetaka mtu yeyote anione nikizungumza na bosi wangu, lakini hapa ninaona aibu mtu fulani kuniona nikizungumza na Bwana wangu."

88 Hapo akahukumika, akalivua vazi lake la kijicho, na chuki, na ugomvi, akaanguka kifudifudi, na kulia mbele za Mungu, mpaka Mungu akamjaza na Roho Mtakatifu, ndipo jambo fulani likatukia, ndipo akawa tofauti. Akaondoa ugumu ndani yake, jambo fulani lilitukia, kwa sababu aliingia kwenye Utukufu huo wa Shekina, akaingia katika uhusiano na Mungu na ushirika wa Kiungu.

89 Hiyo ndiyo sababu ninapenda mikutano hii ya Full Gospel, unawasikia watu wakilia na kupaza sauti na kumsifu Bwana, kwa sababu wameingia katika ushirika, ushirika wa Kiungu wa Roho Mtakatifu. Mungu . . . Kila unapouondoa huo, umerudi Babeli, na afadhali ujizike mwenyewe. Hiyo ni kweli kabisa.

90 Tunapofikia mahali ambapo tunaondoka kwenye huo Utukufu wa Shekina, hizo sifa za Mungu, ule upako mpya unaovunja vizuizi vyote vya kidini, na kadhalika, na kutufanya mmoja katika Kristo Yesu, huru na hukumu yote, hilo ndilo tunalohitaji usiku wa leo. Hivyo ndivyo kanisa . . . Huo ni ushirika wa Kiungu.

91 Hilo ndilo nimeona katika mikutano hii ni mahali ambapo wanaume na wanawake, hawaninii . . . hawaoni haya, hawaionei haya Injili, wako tayari kushuhudia, kuimba kuihusu, kupaza sauti juu yake. Hata nimewasikia wakinena kwa lugha, mara

moja moja. Siwasikii sana tena, lakini mara moja moja wanafanya hivyo.

92 Loo, kamwe msiipoteze hiyo. Kama mkiipoteza hiyo, kufikia mahali ambapo mnaona aibu kuingia katika uhusiano na Kristo! Hebu akae ndani yako, Mungu ndani ya mwanadamu, akijitambulisha Mwenyewe kwa watu kwa Roho Wake, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa kipekee, wasio wa kawaida, tofauti na walimwengu, waliotakaswa kwa Damu na kutengwa na mambo ya ulimwengu. Amina. Hayo ni mahubiri ya kizamani, ya vivi hivi, bali yatamwokoa mtu na dhambi, yatamsafisha mtu na kuwafanya kiumbe kipya katika Kristo Yesu. Haitakupaka chokaa, bali itakuosha ukawa mweupe. Itakuondolea aibu yote, itakuondolea soni.

93 Nimemwona maskini mwanamke mmoja mwenye haya sana, mtu wa bima akija mlangoni, angekirudisha nyuma kichwa chake, hebu ashuke aende madhabahuni na kuingia katika ule Utukufu wa Shekina wa Mungu, atasimama pale na kushuhudia hata viezeko juu ya nyumba vitatikisika. Hakika. Kwa nini? Yuko Mbele za Mungu, amekutana na Mtu fulani aliye halisi, maisha yamekuwa kitu kipya, wala hayajatishiwa tena na ulimwengu, kwa sababu yuko katika ushirika wa Kiungu na Kristo. "Kwangu mimi kuishi ni Kristo," alisema Paulo. Hilo ndilo ninaloita la kiroho halisi.

94 Sasa, huwezi kufanya hivyo kwa kanuni zako za imani. Huwezi. . . Kanuni za imani kamwe hazitairidhisha nafsi yenye njaa. Hizo ni sawa, sina neno dhidi yazo, lakini tunachohitaji siku hizi ni ushirika wa Kiungu, kuna njia moja tu ya kuupata, kupitia kwa Damu, kuingia katika Utukufu wa Shekina.

95 Katika Agano la Kale kuhani mkuu aliingia mara moja kwa mwaka, mara moja kwa mwaka, na hiyo, amebeba damu mbele zake, alikuwa ametiwa mafuta. Loo, ninapenda kusoma jambo hilo, jinsi alivyotiwa mafuta na—na mafuta ya kupaka. Ninaamini Daudi alilia, "Ni vema jinsi gani ndugu kukaa pamoja, kwa umoja! Ni kama mafuta ya kupaka ya thamani yaliyokuwa kwenye nde—ndevu za Haruni, yakashuka hata kwenye upindo wa vazi lake."

96 Mafuta hufanya mambo yaende kirahisi, laini. Mwajua, wakati mtu anapopakwa mafuta kwelikweli na yuko tayari kwa ajili ya Mungu, yeye ni mwepesi tu. Unajua wakati yeye si mwepesi, yeye huketi nyuma akiwa mgumu sana, mwajua, ninii tu, loo, sijui mimi, kama tu ninii . . .

97 Daima nilimhurumia nyumbu. Nyu—nyu—nyumbu alikuwa ndicho kitu kipumbavu kuliko vyote nilichowahi kuangalia, unaweza kumpigia mbinja, umwite, naye ataketi tu na kuyanyosha hayo masikio makubwa, akuangalie. Hajui unyenyekevu kama farasi ajuavyo, mnaona, ha—ha—hana

ujasiri kiasi hicho. Na jambo lingine, nyumbu, ha—hajui alikotoka.

98 Kamwe usiseme Mungu alimfanya nyumbu kamwe, mwanadamu ndiye aliyefanya hivyo. La. Usimtie Mungu hatia ya jambo kama hilo. Huo ulikuwa ni uzao mtambuka, fa—farasi jike pu—punda wa kiume, lakini kamwe usi—usimsingizie Mungu hayo kamwe. Mungu asingefanya jambo kama hilo. La, bwana.

99 Mwajua, napenda farasi mzuri, ukoo safi. Mwajua, farasi mrembo, ukoo safi, yeye kweli ni mzuri, naye anajua baba yake alikuwa ni nani, anajua mahali mama yake alipokuwa, anajua mahali hasa anaposimama. Lakini maskini nyumbu hajui baba yake alikuwa ni nani, mama yake alikuwa ni nani. Na hapa kuna jambo lingine kulihusu: Hawezi kujizaa tena, ameangamizwa maishani.

100 Inanikumbusha mengi ya . . . Inanikumbusha watu wengi wanaojiita Wakristo, wanaozungumza juu ya Damu ya Yesu, nao wanaketi huku wametega masikio yao, wameketi pale kama wenye macho ya kunguni, hata hawajui wito huo unamaanisha nini, hiyo ni kweli, hujui baba yako alikuwa ni nani ama mama yako alikuwa ni nani.

101 Lakini ninakwambia, kama umewahi kuingia chini ya ushirika halisi, wa Kiungu, ukabatizwa kwa Roho Mtakatifu, unajua Baba yako alikuwa ni Nani, unajua mahali unaposimama. Unaijua Damu iliyokusafisha, unamjua Roho Mtakatifu aliyekuzaa na kukupa Maisha mapya, unajua unakotoka, unajua Baba yako ni Nani. Tuna dini nyingi sana za nyumbu siku hizi, naamini, kweli ni—ninaamini, bila aibu yoyote.

102 Kuhani mkuu aliingia mara moja kwa mwaka, mara moja kwa mwaka, akiwa na damu mbele yake, na kuabudu katika Utukufu wa Shekina, amepakwa mafuta kabisa, loo, napenda hilo, amepakwa mafuta, akitembea. Naye alikuwa amevaa mavazi ambayo yalikuwa na komamanga na kengele, naye ilimbidi kutembea na hizo kwa hatua, iliyocheza, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana. Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana,” akienda huku ameitanguliza damu.

103 Ni picha nzuri jinsi gani ya Kanisa siku hizi! Kuingia kwenye . . . Nanyi mnajua sababu ya yeye kuzitengeneza hizo kengele? Watu waliokuwa nje hawakujua kama alikuwa hai au la, isipokuwa awe anapiga kelele. Nakwambia, ndugu! Hmm! Kanisa lililokufa, ambalo halipigi kelele yoyote, ah, jambo fulani limetukia, naam, bwana, hawajaingia mle katika Patakatifu pa patakatifu. Mungu ni . . .

104 Kila mahali unapomwona Mungu, unapata kelele nyingi sana. Ni kweli kabisa. Wakati Yesu alipoingia Yerusalemu, walivunja mitende, hao wakulima wadogo wa Galilaya

wakaanza kuimba, "Hosana, kwake Yeye ajaye katika Jina la Bwana!"

Baadhi ya hao Mafarisayo wakasema, "Loo, hilo hufanya baridi ipande mgongoni mwangu. Huko ni kukufuru. Loo, usifanye hivyo. Wafanye wanyamaze."

105 Yesu alisema, "Wakinyamaza, miamba itapiga kelele mara moja." Jambo fulani halina budi kutukia wakati Kristo anapoingia. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

106 Lakini aliipeleka damu kwenye kiti cha rehema. Na yeye pekee ndiye angeweza kuingia mara moja kwa mwaka. Lakini wakati Yesu alipokufa kwenye Siku ya Upatanisho, Yeye alilipasua pazia vipande viwili. Si kuhani mkuu tu, bali yeyote atakaye anaweza kuja wakati wowote katika Utukufu wa Shekina wa Mungu kwa ubatizo wa Roho Mtakatifu, aingie katika ushirika halisi wa Kipentekoste, amina, aingie mahali fulani Mbele za Mungu, ambapo nguvu za Mungu hutusafisha na udhalimu wote. Tunakuwa viumbe vipya katika Kristo Yesu. Roho Mtakatifu anatushukia, na kurudi nyuma kwetu kwote na aibu, tunakuwa katika uhusiano na Mungu.

107 Je, Kanisa si ni Bibi-arusi? Vema, hivi Bibi-arusi hapaswi kuwa akiwazaa watoto wakilia, "Abba, Baba"? Kuna shi—shida gani? Si ajabu hatuwezi kujizaa wenyewe tena kama tukiwahi kuuondokea huo Utukufu wa Shekina, uondoke humo wala hujui baba yako ni Nani, hujui mama yako ni nani, kutoka chini ya Damu, wajukuu wa Kipentekoste, kama David duPlessis alivyowaita. Mungu hana wajukuu wowote. La, bwana, Mungu anao tu wana.

108 Baadhi yenu ni kama nilivyosema hapa siku moja, tulikuwa tukizungumza juu ya Daudi, kasema, "Watu wanaingia, Wamethodisti waliingia, wakazaliwa wana wa Mungu, halafu watoto wao, wanawapeleka kanisani, na vema, 'Kwa sababu nilikuwa Mmethodisti, basi watoto wangu ni Wamethodisti.'" Sasa, hao kweli si watoto, hao ni wajukuu, mnaona.

109 Lakini sasa, Mungu hana wajukuu wowote. Kila mwanamume, kila mwanamke, kila mvulana, msichana hana budi kupata tukio la kuingia katika Patakatifu pa patakatifu na kuzaliwa mara ya pili. Ni vibaya sana kanisa la Kipentekoste linakuwa hivyo, pia, tuna baadhi ya wajukuu wa Kipentekoste. Hebu niwaambie, Mungu hana wowote, kanisa linao, bali Mungu hana. Kila mtu amjiaye Mungu hana budi kupitia kwa Damu. Kila mvulana, kila msichana hana budi kutambua ya kwamba Kitu fulani kiliwatangulia kipate kufa kwa ajili yao kabla hawajaweza kuingia kwenye Utukufu huo wa Shekina, wawe safi kutokana na maisha ya dhambi, na kuwa viumbe vipya katika Kristo Yesu. Amina.

110 Jinsi alivyoingia katika mahali hapa patakatifu, Patakatifu pa patakatifu kutoa damu hii! Ayubu, kile Kitabu cha kale

kuliko vyote katika Biblia, hata kabla Mwanzo hakijapata kuandikwa, Ayubu aliishi duniani. Nanyi mnamkumbuka Ayubu, shida zake zote, majaribu yake yote, na marafiki zake hata wakimshtaki, rafiki zake wakimpinga, hata hivyo, Ayubu alidumisha a—a—ahadi ya Mungu, alidumisha ushirika katika saa za majaribu, hata akalia, akasema, "Najua Mkombozi wangu yu hai!"

111 Alipokuwa akiteseka na hata mke wake akasema, "Ayubu, kwa nini usimkufuru Mungu ufe?" Ayubu alikuwa chini ya damu, alikuwa ametoa dhabihu ya kuteketezwa, ambapo alijua alikuwa mwenye haki, kwa sababu hilo ndilo Mungu alilohitaji, alikuwa amekuja chini ya damu na alikuwa na ushirika wa Kiungu pamoja na Mungu, hata katika saa za mwisho za majaribu yake makuu, alilia, "Ajaponiua, hata hivyo nitamtumainia!" Amina.

112 Huo ndio kanisa linahitaji leo, ni ushirika wa kujua-hivyo chini ya Damu ya Bwana Yesu Kristo, hata mauti hayawezi kuutia giza.

113 Nimesimama kando ya kitanda chao na kuwaona wakifa kwa kupeana mikono baridi; nimewaona wakisimama pale na kufa, wakipiga makelele ya sifa za Mungu, kwa sababu walikuwa na ushirika, walijua mahali walipokuwa wamesimama. Loo, jinsi ningeweza kupitia tukio la kujua, la matukio ambayo nimeona kwa watu, jinsi wao . . .

114 Kamwe, kamwe usijaribu kumfikia Mungu, chochote kingine ila chini ya ushirika, chini ya, ama, kufanya ushirika na Mungu, ila chini ya Damu. Hiyo ndiyo njia pekee aijuayo Mungu, hiyo ndiyo njia pekee atakayotambua Mungu. Lazima kwanza uoshwe kwa maji ya Neno, kisha utakaswe kwa Damu, halafu uingie katika Utukufu wa Shekina, uingie mle, katika ushirika, ndipo unajua mahali unaposimama.

115 Danieli, mwingine aliyekuwa amekusudia moyoni mwake asingejitia unajisi kwa chakula cha mfalme wakati alipopelekwa Babeli. Alidumisha ushirika wake mbele ya simba waliokuwa tayari kumwua, hata hivyo Danieli alishikilia ushirika wake, ndipo Mungu akamtuma Malaika, na kusimama karibu naye usiku huo, na kuyapofusha macho na kufunga kinywa cha simba, kwa sababu Danieli alikuwa na ushirika na mambo ya Kimbinguni. Danieli alikuwa na ushirika na Mungu wa Mbinguni, kwa sababu alikuwa chini ya damu, hivyo ndivyo alivyodumisha msimamo wake.

116 Wale wana wa Kiebrania, moja kwa moja katikati ya ile tanuru ya moto, haidhuru ungewafanyia nini, huwezi kuunguza ushirika huo utoke ndani yao. Huwezi kuwatupa chini ya majaribu ya kutosha kuwafanya waukane.

117 Mtu ambaye amewahi kuwa chini ya Damu ya Yesu Kristo na akajazwa na Roho Mtakatifu, pepo wote kuzimuni wasingeweza

kuuondoa kwake. Anajua mahali anaposimama...?...Najua unafikiri nina kichaa, nikizungusha mikono yangu, lakini kama ungejisikia kama nilivyojisikia, ungeruka kitini mwako na kufanya jambo lile lile.

118 Lakini sikiliza, ndugu, mtoto mchanga anayezaliwa, wala halii, hatoi sauti ya kilio, mtoto huyo ana kasoro, amezaliwa akiwa amekufa. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo shida ya ninii yetu, makanisa mengi kupita kiasi siku hizi, watu wengi kupita kiasi wanajiita Wakristo, wanazaliwa wakiwa wamekufa, kuzaliwa wafu, haina faida. Wanachohitaji...

119 Unajua daktari hufanya nini wakati mmoja hatoi sauti ya kilio? Anamnyanyua, na kumpindua, anampiga-piga kidogo vizuri, ndipo anapiga kelele. Hilo ndilo kanisa linalohitaji siku hizi, ni ubatizo mwingine mzuri, wa kale, wa Roho Mtakatifu, kutikiswa kwa kanisa, mpaka utaupiga ulimwengu wote utoke ndani yake, ulirudishe kwenye baraka halisi za Kipentekoste, mhubiri halisi ambaye atasimama na kuichukua Injili na kuipiga dha—dhahabu, na kama vile wapigaji wa kale walivyokuwa wakifanya.

120 Wangeipiga hiyo dhahabu, na kuipindua, na kuipiga mpaka takataka yote ikatoka ndani yake. Alijuaje ilikuwa tayari? Wakati alipoweza kuona uakisi wake mwenyewe ndani yake, ndipo alijua hiyo dhahabu ilikuwa tayari, takataka ilikuwa imetoka ndani yake. Hivyo ndivyo Roho Mtakatifu afanyavyo kwa Neno, Anaupiga ulimwengu wote utoke Kanisani, mpaka uakisi wa Yesu Kristo uonekane Kanisani ndani ya watu, wakati Mungu anapoweza kuona uakisi wa nguvu Zake, kama alivyofanya kwenye Siku ya Pentekoste, wakati alipomshusha Roho Mtakatifu, nazo nguvu za Mungu zikawalewesha watu kama divai mpya.

121 Waliposema, "Ati nini? Watu hawa wamelewa kwa mvinyo mpya?"

122 Yeye alisema, "Hili ni lile lililonenwa na nabii Yoeli, 'Itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili, na wana wenu na binti zenu watatabiri. Nitaonyesha mambo ya ajabu katika mbingu juu, na katika dunia chini ishara, na Nguzo za Moto, na moshi, na mvuke, itakuwa kabla haijaja ile siku iliyo kuu ya Bwana, siku iliyo kuu. Kila atakayeliitia Jina la Bwana ataokoka.'"

123 Tunachohitaji leo hii ni kupigwa, Injili kurudi kanisani kulinyosha kanisa kulitoa kutoka kwenye upotovu lililomo ndani, na kurudi chini ya ushirika wa Damu tena katika Utukufu huu wa Shekina, liingie katika tukio la Kipentekoste kama lilivyofanya huko nyuma miaka mingi, mingi iliyopita, kama tulivyokuwa tukifanya miaka mingi iliyopita. Tunachohitaji kama tulivyofanya katika siku za John Wesley, huko nyuma kabisa katika siku za Calvin, Knox, huko nyuma kabisa,

kotekote hata Pentekoste, tunachohitaji ni uhusiano tena, na Mungu, mpaka watu wako tayari kujifia wenyewe katika chumba cha siri pamoja na Mungu, mpaka Uhai mpya utakapotokea, mpaka wawe kiumbe kipya.

124 Hebu mtu afanye hivyo, kama yeye ni maskini mwoga, atatoka na kuwavuta watu. Kwa sababu gani? Amekuwa katika uhusiano wa Kiungu pamoja na Mungu katika chumba cha siri akiwa peke yake, yeye na Mungu, ametiwa mafuta, naye akaingia mle huku machozi yakitiririka mashavuni mwake, na kusema, "Mungu, nipe Roho Mtakatifu. Sijali kama itagharimu mke wangu, watoto wangu, rafiki yangu wa kike, ninii yangu . . . chochote nilicho, nijaze tu, Bwana, mpaka ninapoweza kusimama katika Uwepo Wako na kuhisi Utukufu wa Shekina ukitenda kazi, ukiongezeka juu yangu na kupitia kwangu."

125 Wazieni, wakati huyu Bw. Iverson, baba yake Ned, alipoandika wimbo ule maarufu, *Roho Wa Mungu, Tenda Kazi Ndani Yangu*, hilo ndilo tunalohitaji. "Tenda upya, nishukie, Bwana." Simama hapo mpaka Mungu akuingize kwenye Patakatifu pa patakatifu, afunge mapazia nyuma yako, na kuufungia ulimwengu nje, na kukufungia pamoja na Kristo mpaka uwe hujali ni nani aliye karibu, chochote kile kuhusu hilo, unatembea katika Roho, ukiongozwa na Roho, ukifanya mambo ambayo Roho angetaka ufanye, ukisema yale Roho aliyokujalia kusema, hapo ndipo utakapoingia katika ushirika wa Kiungu. Mungu na amjalie hilo kila mtu. Naam.

126 Wale wana wa Kiebrania, moja kwa moja katikati ya ile tanuru ya moto, wangali walidumisha ushirika wao. Ile tanuru ya moto haikuuzuia, bila shaka haikuuzuia. Wangali walikuwa wakifanya ushirika kadiri walivyowahi kufanya.

127 Maskini Stefano, baada ya kuja chini ya Damu, alisimama pale na kuhubiri mpaka uso wake ukaangaza kama malaika. Siamini uliangaza kama moja ya nuru hizo, la hasha. Malaika si . . . sio lazima sikuzote amaanishe nuru inayoangaza. Malaika ni mjumbe, mtu anayejua wanalozungumzia. Ninaamini wakati Stefano aliposimama pale asubuhi hiyo kwenye lile Baraza la Wazee, walipomkamata, wakijaribu kumhukumu, na kadhalika, yeye alisema, "Ni nani kati ya baba zenu ambaye hajamhukumu Roho Mtakatifu, ama kumkataa? Ni yupi kati yao ambaye hakufanya hivyo?" Kisha akasema, "Enyi wenye shingo ngumu, msiotahiriwa moyoni wala masikioni," akijua ingegharimu maisha yake.

128 Alijali nini? Alijua alichokuwa akizungumzia. Kwa nini? Alikuwa amekuja chini ya ile Damu, na alikuwa huko juu kwenye Pentekoste, naye alikuwa chini ya Utukufu wa Shekina, wala hakujali yale mtu yeyote aliyosema. Mauti hayakumaanisha chochote kwake. Alikuwa na hakika sana, na kujazwa na Roho sana, hata wakaanza kumshambulia na

kusaga meno yao na kuvunja kichwa chake kwa mawe, na kadhalika, namna hiyo. Hata mauti hata hayakuficha ushirika wake, aliinua mikono yake na kusema, "Namwona Yesu."

129 Amina. Whiu! Sasa, hamwamini Wabaptisti hupaza sauti? Nitawaonyesha katika dakika moja. Hebu nikwambie ndugu, hata mauti hayangeweza—hayangeweza kuuficha, mauti hayangeweza kufanya lolote. Usingeweza kumficha kutoka kwenye ushirika, kwa sababu bado alidumisha ushirika huo mkamilifu pamoja na Kristo, hata wakati mawe yalipokuwa yakipigapiga kichwa chake. Yeye. . .

130 Naye Paulo akisimama pale, ilikuwa ni Sauli wakati huo, akishikilia mavazi yake, akiliangalia, kamwe halikumwacha. Aliona ya kwamba mtu huyo alikuwa na Kitu fulani, ingawa alikuwa amejaa sana kanuni za imani, na theolojia, na upuuzi aliyojifunza, hata alimwangalia mtu huyo, naye akaona mtu huyo alikuwa na *kitu fulani* ambacho kanuni zake za imani hazikutoa. Aliona utukufu wa Mungu usoni mwake wakati—wakati Stefano alipoangalia juu, na kusema, "Ninamwona Yesu, amesimama mkono wa kuume wa Mungu," angali akifanya ushirika katika saa ya kufa kwake, kwa sababu alikuja kwa njia iliyopangwa na Mungu, kwa Damu ya Yesu Kristo, naye alikuwa ameingia katika Utukufu wa Shekina, ambako kulikuwa na ushirika halisi, ushirika halisi, sifa na nguvu za Mungu.

131 Warumi 5:1 ikisema, "Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, tuna amani kwa Mungu." Ushirika umerejeshwa. Loo, ninapenda hilo! Ushirika pamoja na Mungu, amani imerudishwa. Jinsi gani? Kwa Damu ya Bwana Yesu.

132 Katika mji wangu mwenyewe, huko Louisville, Kentucky, miezi michache iliyopita, kulikuwako na mzee mmoja kule, walidhani alikuwa tu ni maskini ombaomba, a—angesambaza vitini na kadhalika huko chini mtaani. Naye alikuwa akivuka siku moja. Aliishi katika kibanda kidogo cha kale huko chini karibu na sehemu duni ya mji kule, katika kile tunachokiita Haymarket, naye alikuwa, aliishi huko chini, bali alifanya kazi kubwa, akizunguka huku na huku akisambaza vitini vidogo. Ni kweli, nguo zake sikuzote hazikuwa nadhifu jinsi ninavyodhani zingeweza kuwa, yeye alikuwa ni maskini kapera.

133 Basi alikuwa akivuka barabara siku moja, ndipo motokaa ikamgonga, na kuninii tu. . .Mimi. . .ilionekana kana kwamba kila mfupa ndani yake ulivunjika, likafingirika moja kwa moja juu yake. Nao wakampeleka kwenye gari la kuchukulia wagonjwa, gari la kuchukulia wagonjwa la polisi, na kumpeleka kule kwenye hospitali fulani.

134 Ndipo wakaanza kumchunguza, hospitali ya mji, wakaichunguza mifupa yake, na mifupa mingi sana, hao, nao wakamwekea eksirei, ndipo wakaona kwamba alikuwa amevunjika kabisa. Basi madaktari wakaenda kufanya baraza

dogo, ushirika mdogo miongoni mwao, kwenye kona moja, walidhani huyo mzee alikuwa amezirai, wakasema, "Vema," hao madaktari wakafikia uamuzi huu, "haistahili muda wetu. Hata hivyo, yeye si kitu ila ombaomba tu, wala hamna pesa ndani yake. Kwa hiyo yeye si kitu ila mzururaji tu, kwa hiyo kwa nini tupoteze muda wetu hapa, siku nzima, tukijaribu kumhudumia maskini ombaomba huyo?" Nao walidhani hapakuwapo na . . . Waliamua tu kumfunika tena, na kumwacha aende.

135 Lakini walipoenda pale, hakuwa amekufa kama walivyodhania. Akasema, "Hebu kidogo, enyi waungwana," akasema, "Nina thamani fulani, pia!" Akasema, "Nilikuwa wa thamani sana, hata Mungu akamtuma Mwanawe apate kufa mahali pangu na kunipa neema na ushirika pamoja Naye." Akasema, "Miaka hamsini iliyopita nilikumbatia hilo moyoni mwangu," ushirika halisi pamoja na Mungu, akasema, "na sasa hivi ni mtamu kuliko ulivyowahi kuwa maishani mwangu mwote."

136 Kasema, "Hakika, nina thamani fulani, Mungu alinipenda sana hata akamtoa Mwanawe kwa ajili yangu. Naye aliimwaga Damu Yake ili niweze kuingia katika ushirika pamoja Naye katika mateso Yake, na katika Uwepo Wake." Naye akasema, "Nimeudumisha huo miaka hii yote, na sasa ni mtamu kuliko ulivyowahi kuwa." Mnaweza kuwazia aibu nyusoni mwa hao madaktari wakati huo.

137 Hakika una thamani fulani, kila mmoja wenu ana thamani fulani, Mungu aliutoa Uhai Wake kwa ajili yako. Kwa nini huwezi kutoa wako kwa ajili ya Wake? Kwa nini huwezi kujitolea wewe mwenyewe na wakati? Njoni kabisa. Kama ukikaa mbali . . . Kama—kama huji kwa mtazamo mzuri, sasa, ukienda tu na kuanza, kufungua ukurasa mpya, hilo halitafaa kitu, huna budi kuja kwa njia ya Mungu, uje chini ya Damu, kisha uingie katika Utukufu wa Shekina Mbele za Mungu, ndipo unaweza kumwabudu Bwana Mungu, hakika.

138 Yapata miaka elfu moja mia tisa iliyopita, huko Kalvari, hebu na tuchukue mtazamo mdogo kwa dakika chache tunapopita, ilikuwa asubuhi moja ya kutisha. Loo, hapakuwapo na asubuhi, wala haitakuwako kama hiyo kamwe. Kulikuwa na kesi asubuhi hiyo, kesi ya dhihaka, mahakamani, na Mtu asiye na hatia alikuwa amehukumiwa.

139 Nami naona sasa, ninasikia kitu fulani cha kale kikigongagonga barabarani, kikielekea Kalvari. Na ninapoangalia, kulikuwa na Jamaa mdogo, Biblia ilisema hapakuwapo na uzuri hata tumtamani, alikuwa na msalaba mabegani Mwake, nayo Damu ikafanya michirizi mgongoni Mwake, na ta—taji ya dhihaka ya miiba usoni Mwake, na mate ya askari katili, walevi yakining'inia usoni mwake, akiburuta

mtaani, msalaba wa kale ukizivuta alama za miguu zilizojaa damu ya Mbebaji.

140 Anapoanza kupanda mlimani, ninaona vazi Lake likiwa limelowa Damu, ikigongagonga kwenye pande za mguu Wake, tamasha ambayo hakuna mtu aliyepata kujua maana ya hilo angeweza kuiangalia na kubaki vile vile. Huyo hapo.

141 Loo, ibilisi daima alimtilia shaka, ibilisi alidhani Yeye alikuwa tu ni nabii. Ibilisi alikuwa na hakika wakati huo, ya kwamba huyo alikuwa tu ni nabii, kwa sababu, "Mungu angewezaje kumwacha mtu amtemee mate usoni Mwake? Mungu angewezaje kamwe kupigwa aka—akawa tepetepe?"

142 Mbona, ilikuwa ni sababu ile ile isingeweza kuwa ni nabii, isingeweza kuwa ni Malaika, ilibidi iwe ni Mungu. Ni nani aliyekuja kumtafuta mtoto Wake aliyepotea katika bustani ya Edeni? Je, alimtuma Malaika? Je, alimtuma nabii? Alikuja Mwenyewe. Hivyo ndivyo Mungu alivyokuja akidhihirishwa katika mwili katika Utu wa Mwanawe, Yesu Kristo.

143 Huyu hapa anapanda kilima, akiuvuta msalaba. Ndipo huyo nyuki wa mauti akaanza kulia karibu Naye, akisema, "Mimi—mimi, mwajua, nilimwona *kule* juu, alininukulia Maandiko fulani, lakini nina hakika sasa, yeye si kitu ila mwanadamu, kwa sababu, angalieni, je, Mungu angeweza kumwacha mtu amtemee mate usoni Mwake na apite nayo?"

144 Alifanya hivyo kwa ajili yako. Alifanya hivyo, haikumbidi kufanya hivyo, bali alifanya hivyo kwa ajili yangu na kwa ajili yako. Alifanya hivyo apate kututakasa na kutusafisha na dhambi, huenda akatupa mfano wa jinsi ya kuwa mnyenyekevu, na jinsi ya kuishi vizuri, jinsi ya kutoa shavu lile lingine, ama kuenda maili ya pili, ama—ama kumpa koti ndugu aliyelihitaji. Alifanya yale dini iliyokuwa, dini ya Yehova, Yeye—Yeye—Yeye alikuwa nayo ndani Yake.

145 Naye huyo hapo, akipanda kilima. Ninaweza kumwona nyuki manyoya yule wa kale wa mauti, akimzunguka-zunguka, akimwangalia vizuri, kasema, "Angalieni pale. Je, Mungu angeweza kuwa hivyo? Huyo anaweza kuwa ni Imanueli? La hasha, haingeweza kuwa, Yeye kamwe asingemwacha mtu amtemee mate usoni Mwake, na kumvika taji ya dhihaka ya miiba kichwani Mwake, na kumpa fimbo bandia ya kifalme mkononi Mwake, na kuupiga mgongo Wake ukawa kama mchicha. Mnajua huyo si kitu ila nabii, amenisumbua sana, kwa hiyo bila shaka nitampata katika dakika chache pale Kalvari."

146 Hebu nikwambie, ndugu, wakati alipopiga kelele na kumchoma pale Kalvari, jambo fulani lilitukia. Wakati alipouchomelea mwiba huo katika mwili wa Imanueli... Mnajua wakati nyuki anapouma ka kina, yeye huuchomoa mwiba wake anapokuja. Basi wakati alipouchomelea wakati

huo, alimchoma aliye zaidi ya nabii, alimchoma Imanueli. Ilikuwa ni kitu gani? Aliacha mwiba wake mle ndani.

147 Leo hii, kwa Mkristo mwaminio anayekuja chini ya ile Damu aliyoimwaga pale Kalvari, chini ya ushirika wa Kiungu, ule ushirika halisi, wa Injili yote, wa Kipentekoste, pamoja na baraka za Kipentekoste, na ishara za Kipentekoste, na maisha ya Kipentekoste, sifa za Kipentekoste, unapokuja chini ya huo, mauti hayana mwiba tena, yanaweza kunguruma na kunguruma.

148 Namjua Myahudi katili, mwenye pua iliyopinda, wakati mmoja, mwenye uchungu na asiyejali, alimpiga mawe Stefano, alikuwa akienda zake Dameski siku moja, naye akaanguka chini ya nguvu za Mungu. Nini kilitukia? Alifikia mahali pale mpaka akaingia katika ushirika huo wa Kiungu pamoja na Mwana wa Mungu.

149 Basi siku moja huko Rumi walikuwa wakijenga bloku la dhabihu wapate kukata kichwa chake, kwa ajili ya mauaji ya hadharani chini ya serikali ya Kirumi, basi alipokuwa tayari kufa, nyuki huyo alishuka na kuanza kuvuma karibu naye. Lakini mnajua kile alichosema, alisema, "Ee nyuki, uko wapi mwiba wako? Ewe kaburi, u wapi ushindi wako? Lakini Mungu na ashukuriwe, atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo."

150 Ilikuwa ni kitu gani? Hata katika saa ya kufa kwake, bado alishikilia ushirika huo aliokuwa ameupata huko juu katika baraka hiyo ya Kipentekoste.

151 Kila mmoja wa wanafunzi wa Kipentekoste aliyekuwa pale juu, alidumisha ushirika huo moja kwa moja kupitia majaribu, dhiki, hakuna kitu kingaliweza kuwatenganisha na upendo wa Mungu uliokuwa katika Kristo.

152 Na leo, kuna msingi mmoja tu wa ushirika halisi wa kweli, ushirika huo ni ushirika wa Injili yote. Wakati mtu amepitia kwenye maji ya farakano, akaitambua Damu kwa ajili ya utakaso, na kuingia katika Utukufu wa Shekina, basi uko katika ushirika halisi, wa kweli wa Kipentekoste, wa Injili yote, ndipo huionei haya Injili ya Yesu Kristo, kwa maana ni uweza wa Mungu uletao wokovu, kwa kila aaminiye.

60-0630 Mwongozo Uliotolewa Na
Mungu Wa Kuuendea Ushirika Wa Kiungu

Abundant Life Building

Tulsa, Oklahoma Marekani

SWAHILI

©2026 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org